OR-TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA LUSHOTO
SHULE YA SEKONDARI KISABA
S.L.P 206 LUSHOTO
MAAGIZO YA WANAFUNZI WANAOJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

JINA: ……

Ninayo furaha kukujulisha kwamba umechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Kisaba kama kidato cha kwanza kwa mwaka 2021

Tafadhali zingatia maelezo yafuatayo;

1. Shule inafunguliwa tarehe 11/01/2021,Ni muhimu kufika siku hiyo.Mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe 18/01/2021.Iwapo hutaripoti taratibu za kisheria zitachukua mkondo juu wako.

2. SARE YA SHULE

(a) WAVULANA

(i) Suruali mbili, rangi ya kaki moja (1) na rangi dark green moja (1) zisizobana.

(ii) Mashati mawili (2) meupe mikono mifupi.

(iii) Sweta rangi ya ugoro moja (1) na dark green moja (1).

(iv) Tai mbili (2) rangi ya kaki moja (1) na dark green moja (1).

(v) Viatu vyeusi vya ngozi na vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi.

(vi) Soksi nyeusi pea mbili (2) au zaidi

(vii) Mkanda wa suruali mweusi au kahawia

(b) WASICHANA

(i) Sketi mbili (2) rangi ya kaki moja (1) na dark green moja (1),linda box,belt ya wastani,ndefu kuvuka goti na kuwezesha soksi kuonekana

(ii) Shati mbili (2) nyeupe za mikono mifupi.

(iii) Viatu vyeusi vya ngozi na vya kufunga kwa kamba vyenye visigino vifupi.

(iv) Soksi nyeupe pea mbili (2) au zaidi zisizo na urembo.

(v) Tai mbili (2) rangi ya kaki moja (1) na dark green moja (1).

(vi) Hijabu mbili (2) nyeupe za kushona zisizo na marembo (kwa wanaovaa tu)

(vii) Sweta rangi ya ugoro moja (1) na dark green moja (1) au zaidi

Kwa wasichana wanaovaa sare ya nusu kanzu (Hijabu)

(i) Blauzi za nusu kanzu mbili (2) nyeupe zenye urefu wa wastani na pana (zisizodhihirisha maungo)

(ii) Suruali rangi ya kaki 1 na dark green 1 zisizobana

(iii) Hijabu nyeupe mbili (2) za kushona zisizo na marembo

(iv) Sweta rangi ya ugoro moja (1) na moja (1) rangi ya dark green au zaidi

3.NGUO ZA MICHEZO

- T.shirt rangi ya bluu moja (1)
- Raba ya michezo pair moja (1)
- Track (suruali ya michezo) nyeusi au bluu yenye ufito mweupe.

NB:Zingatia kwa makini maagizo ya sare ya shule kwa kulinda maadili na nidhamu ya shule,pia sare ni lazima iwe mpya.Sare chakavu haitakubaliwa.

4. VIFAA VYA TAALUMA

(i) Daftari kumi (10) counter book kwaya two au zaidi

(ii) Mkebe (Mathematical set) moja (1)

(iii) Rula moja (1)

(iv) Kalamu za wino,penseli,kifuto

(v) Kamusi (dictionary) ya kiingereza kwa kiingereza (ni muhimu)

5.FOMU MBALIMBALI

(i) Fomu ya taarifa ya mwanafunzi.

Ijazwe kikamilifu na irudishwe shuleni siku ya kuripoti

(ii) Fomu ya kupimwa afya.

Mwanafunzi apelekwe hospitalini na daktari ampime na kujaza taarifa za afya yake katika fomu hiyo.(Ijazwe kwenye hospitali ya serikali au kituo cha afya).

Nakutakia maandalizi mema

…….

MWIKALO,A.P

MKUU WA SHULE

FOMU YA TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1.Jina la mwanafunzi ……..

2. Tarehe ya kuzaliwa ……

3. Jina la mzazi/mlezi ……

4. Anuani ya mzazi/mlezi …….

5. Kijiji …….

6. Shule ya msingi aliyotoka ……

7. Saini ya mwanafunzi ……..

UTHIBITISHO WA MZAZI / MLEZI / MFADHILI

Mimi……mzazi/mlezi/mfadhili wa mwanafunzi mtajwa hapo juu,aliyekubaliana na maelezo.Naahidi kuwa nitakamilisha taratibu zote za shule kila mwanzo wa muhula bila usumbufu wowote na nitamsimamia mwanafunzi huyu kufika shuleni kila siku mpaka atakapomaliza kidato cha nne.Nikishindwa kutekeleza majukumu hayo nichukuliwe hatua kali za kisheria.

Jina…… Saini…….... Tarehe……..

UTHIBITISHO WA MWANAFUNZI

Mimi……naahidi kuwa mwanafunzi mtiifu na mwenye kufuata sheria na taratibu za shule.Nikivunja sheria na taratibu za shule nichukuliwe hatua kali za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa shule.

Jina…….. Saini ……. Tarehe ……

GOVERNMENT OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

KISABA SEKONDARI,
S.L.P 206,
LUSHOTO.

MEDICAL OFFICER,

_____

_____

MR _____

Please examine the above named student that he/she si physical and mental fit/unfit for full time schooling course.

(a)(i) Eye sight_____
(ii)Hearing_____
(iii)Limbs_____
(iv)Speech_____
(v)Venereal disease_____
(vi)Leprosy_____
(vii)Epilepsy_____
(b)Neuroses_____
(c)Other serious disease (mention)_____
(d)Pregnant test_____

Station_____Name_____Signature_____

Designation_____Date_____

SHULE YA SEKONDARI KISABA
KANUNI NA SHERIA ZA SHULE KWA WANAFUNZI

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu sayansi Teknolojia na ufundi nchini. Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo yafuatayo awapo shuleni hapa.

KANUNI NA TARATIBU.

I. Kutii kengele muda wote na kuwahi shule.
II. Heshima kwa walimu, viongozi na wanafunzi wenzie.
III. Kutotoa lugha chafu na za matusi shuleni.
IV. Kutomnyanyasa mwanafunzi mwenzie.
V. Kuhudhuria shule wakati wote.
VI. Kuwa ndani ya eneo la shule muda wote unaotakiwa.
VII. Kutunza na kuhifadhi mali zote za shule.
VIII. Kuvaa sare sahihi ya shule muda wote.
IX. Kutumia lugha ya kiingereza kwa mawasiliano yote ndani ya eneo la shule
X. Ni marufuku mwanafunzi kutumia simu.
XI. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa mapambo kufuga kucha, ndevu na kupaka rangi kucha. Kupaka rangi midomo na kufuga nywele.
XII. Matumizi ya madawa ya kulevya na ulevi kwa ujumla hayaruhusiwi ndani na nje ya shule.
XIII. Mwanafunzi anatakiwa aheshimu wimbo wa Taifa, Bendera ya Taifa na Nembo ya Taifa.
XIV. Mwanafunzi anatakiwa kufuata ratiba ya shule ipasavyo.
XV. Kuthamini kazi apewazo.
XVI. Mwanafunzi anatakiwa adumishe utulivu na ukimya awapo shuleni.

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

I. Uasherati na ubakaji
II. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
III. Kupewa ama kusababishia ujauzito na kutoa mimba.
IV. Kupigana
V. Makosa ya jinai, wizi, na kuvuruga amani.
VI. Kuharibu kwa makusudi mali ya shule.
VII. Kugomea adhabu kwa makusudi.

ZINGATIA:

Uzito wa kosa lolote unaweza kumsababishia mwanafunzi kusimamishwa masomo kwa muda ama hata kufukuzwa shule hata kama kosa hilo halipo katika haya yaliyoorodheshwa.